



Kupakusa mpunga

Kutenga Mpunga

Kutega mpunga kutoka kwenye sehemu zingine za mmea hufanywa na mkono, iwapo mashine za kufanya kazi hii hazipo.

Kulainisha

Kunazo mashine za kulainisha kwenye mashamba madogo sehemu kadhaa nchini.

Matumizi

Mpunga hutumika sana kwa chakula, na pia kuandaa biskiti tamu na mihimili. Maganda na majani makavu yanaweza kutumiwa kama lishe ya mifugo. Ukuzaji mpunga kwa kutumia maji ya mvua ni kazi yenye manufaa ya kifedha na ya kuleta faida.



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Watayarishaji:

Kore W., Onyango G. na Omuga G.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkuu wa Kituo,

KARI-Kibos

S.L.P. 1490-40100

Kisumu

Simu: 020-207182

Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 52 /2008

Shilingi 20 za Kenya

Kilimo cha mpunga kutegemea mvua



Utangulizi

Mpunga hunawiri sehemu zenye joto kuanzia pwani hadi mita 1,700 juu ya bahari. Mpunga huhitaji milimita 400 au zaidi za mvua na mchanga unaolowa maji polepole hadi unalowa vyema.

Mwea na Ahero ndiko mpunga unakokuzwa kwa kunyunyizia kwa ardhi kubwa hali ukuzaji mpunga unategemea mvua katika sehemu zingine ambako aina kadhaa zinakuzwa.

Aina Za Mpunga

Aina mwafaka ni kama Dourado Precoce, NERICA 1, NERICA 4, NERICA 10, NERICA 11. Aina hizi hukomaa kwa siku 60 hadi 120 na kutoa mazao kati ya tani 3.5 hadi 5.5 kila hektari mimea ikitunzwa vyema na mazingira mwafaka.



Mpunga wa NERICA



Vichwa vya mpunga vilivyokomaa

Ukuzaji

Utayarishaji ardhi

Tayarisha kitanda cha kupandia vyema kwa kutumia tingatinga, dume na plau au jembe la mkono.

Kupanda

Kupanda kwenye mistari au vijilima unaweza kutumiwa, kwa udani wa sentimita 2 hadi 3.

Nafasi

Sentimita 25 kati ya michoror kisha kumwaga mbegu (drill) au 25 kwa 15.

Kiasi cha mbegu

Kilo 50 hadi 75 kwa hektari.

Mbolea

Mifuko 2 kwa hektari za TSP au DAP wakati wa kupanda na mfuko mmoja wa CAN kwa kila hektari (bag/ha) baada ya siku 20 na 50 baada ya kumea.

Kupalilia

Ng'oa kwekwe mara 2 hadi 3.

Uzuiaji wadudu na maradhi



Mdudu mvamizi



Ugonjwa wa mpunga

Kuza mimea kama NERICA ambayo hustahimili magonjwa lakini iwapo maradhi yatatokea, tafuta usaidizi kituoni cha kilimo kilicho karibu nawe. Punguza athari za ndege kwa kuwafukuza.

Uvunaji

Vuna mpunga uliokomaa kwa kutumia vifaa maalum yya kukatia (sickles).



Mpunga uliovunwa